1410/206
KISWAHILI
Oct./Nov. 2021
Muda: saa 3

THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

# NATIONAL CERTIFICATE IN SOCIAL DEVELOPMENT

KISWAHILI

**Muda: saa 3**

## MAAGIZO KWA WATAHINIWA

*Mtihani huu una sehemu* ***NNE:***
***insha, ufahamu, matumizi ya lugha na mbinu na vifaa vya kufundisha.***
*Jibu maswali* ***YOTE*** *kwenye kijitabu cha majibu ulichopewa.*
*Ni muhimu sana ufuate maagizo uliyopewa mwanzo wa kila sehemu.*
*Usitoe karatasi yoyote katika kijitabu hiki.*
***Jibu maswali kwa kutumia lugha ya Kiswahili.***

easytvet.com

**Karatasi hii ina kurasa 5 zilizopigwa chapa.**

**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi ya mtihani zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

© 2021 The Kenya National Examinations Council

**Fungua ukurasa**

## SEHEMU A: INSHA (alama 20)

1. Andika insha isiyopungua kurasa mbili wala kuzidi kurasa mbili na nusu juu ya mojawapo ya vichwa vifuatavyo:

(a) Andika insha itakayomalizika kwa maneno

... alijipiga kifua na kuapa ya kwamba angechukua usukani wa maisha yake baada ya kujifunza kutokana na matatizo yaliyompata.

(b) Umuhimu wa simu tamba katika maisha.

(c) Wewe ni nahodha wa timu ya mchezo wa magongo shuleni mwako. Timu yako imeshinda katika mchuano wa mabingwa wa wilaya. Andika ripoti kuhusu mechi hiyo.

(d) Aisifuye mvua, imemnyea.

## SECTION B: UFAHAMU (alama 30)

2. *Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.*

Pindo alipozaliwa katika mtaa wa kifahari wa muthaiga, kule Nairobi, Bw. Atanasi na mkewe, Bi. Sumba walisherehekea si haba. Kwa miaka na mikaka walikuwa wametembea pembe zote za ulimwengu wakisaka mwana. Maadam walikuwa watu na chao, iliaminiwa kwamba wangefaulu. Huku wakitamba na njia, kule kijijini kwao Paukwa, wanakijiji walikuwa na **hisia mseto** kufuatia hali hii ya Atanasi na mkewe. Wapo waliowanyoshea kidole cha lawama wapenzi hawa wakidai kuwa huenda dhiki yao inawaandama kwa kuwa Bw. Atanasi alioa msichana wa kijijini mwao. Hawa waliamini kuwa mradi kwa kina Sumba kulikuwa karibu kama mdomo na pua na kwa Atanasi, basi wawili hawa wana uhusiano wa kidamu. Waliwachukulia kuwa **maharimu**. Wengine walidai kukosa mtoto kwa wawili hawa kulitokana na dhehebu fulani ambalo liliwatunukia mali na kuwanyima uzazi. Wa kuumeni walimlaumu Sumba huku wa kuukeni wakimlaumu Atanasi. Hivyo basi, ujio wa Pindo uliandaliwa karamu ya kukata na shoka. Wanakijiji waliowasengenya wakala, wakanywa na kusaza.

Pindo alilelewa kwa tunu asikose chochoke. Ingawa Bi. Sumba alikuwa mkali kama simba, kwa upande mwingine Atanasi alimdekeza mwanawe wa pekee. Alisajiliwa katika shule ya kimataifa ya Hilcrest. Mbali na kutengewa gari lake la kipekee la kumpeleka shule, aliajiriwa dereva wake mahususi. Watumishi wa nyumbani kwao hawakumpa fursa ya kugusa kazi yoyote mle. Alifuliwa nguo hata zile za siri. Nusura alishwe mwana huyu. Alisafishiwa chumba chake cha kulala pamoja na kutandikiwa kitanda. Ulikuwa mwiko kwa Pindo kutumia malazi kwa siku mbili. Pindo hakukatazwa kutenda alilotaka nyumbani kwao. Hali hii ilimkera sana Bi. Sumba bali Bw. Atanasi hakumpa nafasi ya kufungua kinywa chake kusema lolote. Kufinywa huku

kwa Bi. Sumba kulikuwa arusi kuu kwa Pindo . Alipojaribu kuzungumza, alikatwa kalima na Bw. Atanasi kabla atamke neno. Alijinywea. Sumba alifahamu fika kuwa mchelea mwana kulia hulia yeye.

Kisadfa, Pindo aliendelea vyema katika mitihani yake yote. Kule shuleni, **alivalia ngozi ya kondoo**. Walimu wote walimpenda kwa kuwa alikuwa mwepesi wa kutumika na mcheshi. Mwalimu mkuu, Bi. Nasra aliwakumbusha wanafunzi wengine kuigia mfano mwema wa Pindo. Alimteua Pindo kuwa kiranja msimamizi wa wasichana wote shuleni. Ilikuwa kama tuzo kwa mienendo yake mizuri. Hata hivyo, wahenga walisema kuwa hakuna mchele ukosao ndume na kuwa mgema akisifiwa tembo hulitia maji.

Haikuchukua muda kaba Pindo aanze visanga. Alianza kunyamaza tu. Walimu wakashtuka. Walipotaka kujua sababu ya kimya hiki, Pindo alidai kuwa alihisi uchovu mwilini. Kule nyumbani pia, Bw. Atanasi alikuwa tayari ameyashuhudia mabadiliko haya. Kwa kawaida, alikuwa msichana mchangamfu sana. Alipotoka shuleni, angemwangukia babake na kumkumbatia kwa furaha. Hili lilibadilika akawa anarudi na kufululiza hadi chumbani mwake na kuujifungia. Bi. Sumba naye aliwatazama tu kwani yeye alizoea kupewa salamu za kupungiwa mkono na kuambiwa kwa mbali, 'Hi Mom'. Sumba alikerwa sana na mwelekeo huo. Bw. Atanasi alizongwa na mawazo kutokana na hali hii, akaamua kuchukua hatua. Alikwenda moja kwa moja hadi shuleni ili kujua **mbivu na mbichi**. Alishangaa kupata kuwa Pindo alikuwa amebadilika hata kule. Matokeo yake katika mitihani ya muhula huo yalikuwa yamedorora kiasi cha kutia wasiwasi. Mwalimu mkuu alidai kuwa alikuwa amempa Pindo barua tatu za mwaliko kwa babake kuja shuleni ili wajadili suala hilo. Atanasi akasononeka sana kwani hakuwahi kupata barua hata moja. Kumbe Pindo alizificha barua zenyewe. Hapa ndipo Bw. Atanasi alipofikia uamuzi kuwa mwanawe alihitaji usaidizi wa kitaalamu. Alimwalika daktari wao nyumbani ili kumchunguza mwanawe. Wanasema, ukistaajabu ya Musa, utayaona ya firauni. Bw. Atanasi **aliduwaa** asijue la kufanya ilipobainika kuwa mwanawe wa pekee, Pindo alikuwa ameambukizwa ugonjwa wa kisonono. Atanasi alipigwa na butwaa. Kuchunguza mkosaji, iligunduliwa kuwa alikuwa dereva kuto.

easyelimu.com

**MASWALI**

(a) Ipe taarifa hii uliyoisoma kichwa mwafaka. (alama 2)

(b) Taja sifa moja ya wanakijiji cha Paukwa. (alama 2)

(c) Eleza mambo manne yanayoonyesha kuwa Pindo alidekezwa. (alama 8)

(d) Onyesha ukweli wa methali, mchelea mwana kulia, hulia mwenyewe'. (alama 2)

(e) Taja sifa mbili za Bw. Atanasi. (alama 2)

(f) Walimu walimshukuru Pindo kwa kuwa mwenye kuwajibika. Thibitisha. (alama 4)

(g) Ni kwa vipi Pindo alionyesha tabia ya ujanja? (alama 2)

(h) Taja matokeo matatu kutokana na mabadiliko ya Pindo. (alama 3)

(i) Eleza msamiati huu kama ulivyotumika katika taarifa.

(i) hisia mseto
(ii) maharimu
(iii) alivalia ngozi ya kondoo
(iv) mbivu na mbichi
(v) aliduwaa (alama 5)

## SEHEMU C: MATUMIZI YA LUGHA (alama 20)

*Jibu maswali yote katika sehemu hii.*

3. (a) Onyesha viambishi katika neno hili.

walivyovitumia (alama 2)

(b) Nomino hizi zimo katika ngeli gani? (alama 2)

easytvet.com

(i) baridi
(ii) mpera

(c) Geuza sentensi ifuatayo iwe katika umoja.

Nyinyi mtalipa kodi kwa wenye vibanda. (alama 2)

(d) Taja matumizi ya neno 'vile' katika sentesi zifuatazo. (alama 2)

(i) Mama alinunua vijiko <u>vile</u>.
(ii) Mwalimu alituonyesha <u>vile</u> tunavyofaa kuandika.

(e) Ainisha viwakilishi vilivyopigwa mstari katika sentensi zifuatazo. (alama 2)

(i) <u>Wenyewe</u> walitutumbuiza hadi jioni.
(ii) <u>Chema</u> hupendeza kila mwanadamu.

(f) Kanusha sentensi hii: (alama 2)

Mkulima amevuna mahindi mengi.

(g) Andika maneno yafuatayo katika kauli zilizo mabanoni. (alama 2)

(i) Jigongo (udogo)
(ii) Kijidudu (wastani)

(h) Tunga sentesi moja ukitumia maneno yafuatayo. (alama 2)

fuma, vuma

(i) Tambulisha tamathali za usemi katika sentensi zifuatazo. (alama 2)

(i) Jumba alipigwa akatoa unyende uliotushtua.
(ii) Yeye ni malaika; hupendwa na wote.

(j) Andika methali yenye maana sawa na hii. (alama 2)

Mchumia juani hulia kivulini

**SEHEMU D: MBINU NA VIFAA VYA KUFUNDISHIA** (alama 20)

easytvet.com

*Jibu maswali yote katika sehemu hii.*

4. (a) Wewe kama mwanasanaa mtajika katika kata yako, umealikwa kuwazungumzia vijana wa mtaani kuhusu mbinu za kufaulu katika sanaa ya vichekesho. Andika hotuba yako. (alama 10)

(b) Eleza mbinu utakazotumia kuwashauri vijana kuhusu umuhimu wa kujishughulisha na utunzaji wa mazingira yao. (alama 10)

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.**